

Maseyidi 12 wa Ishmaeli, ni wakina nani?.2)Taa ya Mungu ambayo  
ilikuwa haijazima wakati wa Eli ni ipi?

**SWALI:** Naomba kuuliza watumishi wa Mungu katika Mwanzo 17:20  
anaposema kwa habari ya Ishmaeli atazaa maseyidi 12, hao ndio akina  
nani kwa Sasa?

2) Pia katika 1samweli 3:3 anasema kipindi Samweli anaitwa na Mungu  
taa ilikua haijazimika bado Nia taa gani hiyo? Asante Sana Ni hayo.

---

### **JIBU:**

1. Tusome..

Maseyidi 12 wa Ishmaeli, ni wakina nani?.2)Taa ya Mungu ambayo  
ilikuwa haijazima wakati wa Eli ni ipi?

*Mwanzo 17:18 “Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba  
Ishmaeli angeishi mbele yako.*

*19 Mungu akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa  
kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami nitafanya agano langu  
imara kwake kuwa agano la milele kwa ajili ya uzao wake baada  
yake.*

*20 Na kwa habari za Ishmaeli nimekusikia, nimembariki,  
nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi  
na wawili, nami nitamfanya awe taifa kuu”.*

Neno Seyidi linamaanisha mtawala, hivyo hapo biblia ilimaanisha kuwa  
Ishmaeli atazaa watawala 12.. ambao utaona wakitajwa kwa majina  
katika Mwanzo 25:13

Maseyidi 12 wa Ishmaeli, ni wakina nani?.2)Taa ya Mungu ambayo  
ilikuwa haijazima wakati wa Eli ni ipi?

*Mwanzo 25:13 “Na haya ndiyo majina ya wana wa Ishmaeli, kwa majina yao, na kwa vizazi vyao. Mzaliwa wa kwanza wa Ishmaeli, ni Nebayothi, na Kedari, na Abdeeli, na Mibsamu,*

*14 na Mishma, na Duma, na Masa,*

*15 na Hadadi, na Tema, na Yeturi, na Nafishi, na Kedema.*

*16 Hao ndio wana wa Ishmaeli, na hayo ni majina yao, katika miji yao, na katika vituo vyao, maseyidi kumi na wawili kwa kufuata jamaa zao.*

Katika historia wana hawa wa Ishmaeli walikuwa watu wakuu sana, na ndio chimbuko la mataifa ya kiharabu tunayoyaona sasahivi kule mashariki ya kati.

## **2) Je ni Taa ipi hiyo inayozungumizwa katika 1Samweli 3:1?,**

Tusome.

Maseyidi 12 wa Ishmaeli, ni wakina nani?.2)Taa ya Mungu ambayo  
ilikuwa haijazima wakati wa Eli ni ipi?

*1 Samweli 3:1 "Basi, mtoto Samweli akamtumikia Bwana mbele ya Eli. Na neno la Bwana lilikuwa adimu siku zile; hapakuwa na mafunuo dhahiri.*

*2 Ikawa wakati huo, Eli alipokuwa amelala mahali pake (tena macho yake yalikuwa yameanza kupofuka, hata asiweze kuona),*

*3 na taa ya Mungu ilikuwa haijazimika bado, na Samweli alikuwa amelala katika hekalu la Bwana, palipokuwa na sanduku la Mungu;*

Inadhaniwa kuwa hiyo ni ile taa ya hekaluni, lakini ukitafakari kwa ukaribu, utaona kuwa biblia haikumaanisha ile taa ya hekaluni au ile ya kwenye hema ya kukutania, bali ilimaanisha pumzi au uhai wa Eli, ukikumbuka kuwa habari iliyokuwa inazungumziwa hapo juu ni kuhusu uzee wa Eli, ambapo inasema umri wake ulikuwa umeshaenda sana mpaka macho yake yalikuwa yameshaanza kupofuka.

Biblia inasema..

Maseyidi 12 wa Ishmaeli, ni wakina nani?.2)Taa ya Mungu ambayo  
ilikuwa haijazima wakati wa Eli ni ipi?

*Mithali 20:27 “Pumzi ya mwanadamu ni taa ya Bwana; Hupeleleza  
yote yaliyomo ndani yake”.*

Unaona? Hivyo hapo ilimaanisha kuwa Pumzi ya uhai wa Eli ilikuwa  
bado haijamuacha.

Hiyo ni kutukumbusha pia, kuwa upo wakati na sisi Taa ya Mungu  
itazima ndani yetu. Na kama tunavyojua taa ikizimika huwa kunakuwa  
na giza na sikuzote gizani hakuna shughuli yoyote inayoendelea. Vivyo  
hivyo na siku ambayo kila mmoja wetu atakufa, huko atakapoenda  
hakuna jambo lolote la kimaendeleo atakalolifanya, Hatakuwa na nafasi  
ya pili ya kutubu ikiwa alikufa katika dhambi, hatakuwa na nafasi ya pili  
ya kufanya marekebisho ikiwa alizembea zembea katika masuala ya  
wokovu wake akiwa hapa duniani. Atakachokuwa anasubiria huko ni  
hukumu tu.

*Mhubiri 9:5 “kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa;  
lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana  
kumbukumbu lao limesahauliwa”.*

Maseyidi 12 wa Ishmaeli, ni wakina nani?.2)Taa ya Mungu ambayo  
ilikuwa haijazima wakati wa Eli ni ipi?

Hivyo tunapaswa tujithamini maisha yetu tunamalizaje mwendo tukiwa  
hapa duniani? . Kwasababu huko ng'ambo hakuna nafasi ya pili.

Bwana akubariki.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.

Piga namba hizi: **+255693036618 au +255789001312**

**Jiunge na kundi letu la mafundisho ya Biblia whatsapp kwa  
kubofya hapa > [Group-whatsapp](#)**

### **Mada Nyinginezo:**

*Kiango na Pishi ni nini (Mathayo 5:15)?*

*Kwanini Kuhani wa Mungu Eli alikufa kwa kuvunjika shingo?*

*JE NI LAZIMA KUBADILISHA JINA BAADA YA KUOKOKA?*

Maseyidi 12 wa Ishmaeli, ni wakina nani?.2)Taa ya Mungu ambayo  
ilikuwa haijazima wakati wa Eli ni ipi?

***JE NI LAZIMA KUBADILISHA JINA BAADA YA KUOKOKA?***

*Mafundisho*

**Rudi nyumbani**

Share on:

WhatsApp